

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA  
SHULE YA SEKONDARI YA IGOTA, S. L. P. 154, MAHENGE/ULANGA.**

MZAZI/ MLEZI WA.....TAREHE.....

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGOTA.**

Ninakujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika **SHULE YA SEKONDARI IGOTA mwaka 2021.**

Kauli mbiu ya shule ni JITUME kila mwanafunzi anatakiwa kujenga tabia ya KUJITUMA kwa **MAFANIKIO YAKE KATIKA TABIA NJEMA, TAALUMA NA KAZI.**

**TAREHE YA KUFUNGUA SHULE:**

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** na kila mwanafunzi anatakiwa kufika shulenii siku hiyo kwa usajili.

Mwanafunzi anaporipoti shulenii anatakiwa kuwasilisha;

- ✓ Fomu ya ahadi ya mzazi.
- ✓ Fomu ya ahadi ya mwanafunzi.
- ✓ Fomu ya kupimwa afya.

**MAHITAJI. A: SARE ZA SHULE.**

- ✓ Shati jeupe mikono mifupi (kwa wasichana na wavulana).
- ✓ Sketi (kwa wasichana) iwe ya mshono wa linda box, mbele na nyuma (*ndefu ambayo huachia inchi sita tu (pima hizo nchi sita ukianzia usawa wa ardhi)*, rangi ya damu ya mzee au suruali (kwa wavulana) ya kawaida rangi ya damu ya mzee (*iwe na seleburesheni na turn-up na upana wa mguu wa suruali kwa chini iwe nchi 16*)
- ✓ Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga kwa kamba na kisigino kifupi (kwa wasichana na wavulana)
- ✓ Soksi rangi nyeupe ( kwa wasichana na wavulana)
- ✓ Tai nyeupe yenye *mistari ya rangi ya damu ya mzee*. Fulana (*rangi ya damu ya mzee*), Sweta (*rangi ya damu ya mzee- V-shaped neck*).
- ✓ Wasichana sketi *rangi ya bluu na viatu vya raba* kwa ajili ya michezo
- ✓ Wavulana suruali *rangi nyeusi, bukta na viatu aina ya raba* kwa ajili ya michezo.

**B: VIFAA VYA TAALUMA.**

- ✓ Mkebe mmoja wa vifaa vya Hisabati .
- ✓ Madaftari makubwa yasiyopungua kumi.
- ✓ Begi dogo la kubebia vifaa vya mwanafunzi vya Shule.
- ✓ Kalamu za wino.
- ✓ Ream moja ya karatasi A4 kwa mwaka. (*Huu ni uamuvi halali wa wazazi katika kikao rasmii*)

**ZINGATIA: Sare za Shule na Vifaa vya Taaluma vyote vitakaguliwa ipasavyo siku ya usajili.**

**ASANTE KWA USHIRIKIANO MWEMA**



**PAUL KAJURUNGA JOHN**

**MKUU WA SHULE.**

**HEAD OF SCHOOL  
IGOTA SEC. SCHOOL  
P.O BOX 154 MAHENGE/ULANGA**

**SHULE YA SEKONDARI YA IGOTA  
FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.**

Ndugu Mzazi/ Mlezi, Shule inahitaji kufahamu mambo yafuatayo kuhusu mtoto wako.

- Jina kamili la mtoto .....
- ✓ Tarehe yake ya kuzaliwa .....
  - ✓ Kabilia lake .....
  - ✓ Dini yake .....
  - ✓ Je ana ugonjwa wowote unaomsumbu mara kwa mara? **NDIYO/HAPANA** Kama ndiyo anatibiwa hospitali gani? .....
  - ✓ Anaishi na nani akiwa nyumbani , Mzazi/ Mlezi .....
  - ✓ Jina la mzazi/ mlezi .....
  - ✓ Anuani yake .....
  - ✓ Simu ya mkononi/ nyumbani .....
  - ✓ Simu ya kazini .....
  - ✓ Kazi ya mzazi/ mlezi .....
  - ✓ Sehemu unakoishi kwa sasa .....

**IJAZWE NA MZAZI /MLEZI.**

Mimi ..... **NINAKUBALI/ SIKUBALI** Nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari ya Igota, naahidi kukubaliana na sheria za shule na kumtimizia mahitaji yote mwanangu kabla ya kujiunga na Shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwa mujibu wa sheria ya uendeshaji wa Shule nchini Tanzania.

SAHIHI ..... TAREHE .....

**IJAZWE NA MWANAFUNZI HUSIKA.**

Mimi ..... **NINAKUBALI/ SIKUBALI** nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari ya Igota, naahidi kukubaliana na sheria za shule na kutunza mali za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na shule.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO MWEMA**



**PAUL KAJURUNGA JOHN**

**MKUU WA SHULE.**

HEAD OF SCHOOL  
**IGOTA SEC. SCHOOL**  
P.O.BOX 154 MAHENGE/UJLAHNA

## **SHERIA, KANUNI, TARATIBU ZA SHULE.**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu mtu yejote anayemzidi kwa umri kwa kusimama na kuamkia kwa wakati wote.
2. Kila Mwanafunzi awe mtiifu kwa Walimu na wafanyakazi wasio Walimu.
3. Hutakiwi muda/ wakati wowote kuwa nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya *MKUU WA SHULE AU MWALIMU WA ZAMU*.
4. Ni marufuku mwanafunzi kwenda kwenye nyumba za walimu/ wafanyakazi wasio Walimu bila sababu ya msingi.
5. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo bila kukosa na ni lazima kufanya mazoezi, majoribio na mitihani yote inayotolewa.
6. Wanafunzi wote watanya nywele kwa mtindo wa kawaida (Kunyoa kipara hairuhusiwi).
7. Mwanafunzi atatumia sare maalumu za Shule kulingana na wakati/ Mahali atakapokuwa. Ni marufuku kuva nguo yoyote isiyo sare iliyoruhusiwa.

### **Makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja akitayatenda:**

1. Wizi.
2. Uasherati, Uhusiano wa jinsia moja, kuo au kuolewa, kubaka, kulawiti.
3. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
4. Kutembelea nyumba za starehe au nyumba za kulala wageni.
5. Ulevi wa aina yoyote.
6. makosa ya jinai.
7. Uvutaji wa bangi na madawa ya kulevya.
8. kupiga/ kupigana.
9. kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
10. kudharau bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Wimbo wa shule.
11. kupata ujauzito au kutoa mimba.
12. kusababisha mimba au kumpa mimba msichana/ mwanamke.
13. kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
14. kukataa adhabu kwa kukusudia.
15. kugoma na kuhamasisha mgomo.
16. kumiliki simu, au kutumia simu ya mkononi au kukutwa na simu katika mazingira ya shule.
17. kutohudhuria masomo kwa siku tisini bila taarifa/utoro.
18. kufuga ndevu/ kucha, kupaka rangi kwenye kucha /midomo, kutumia vipodozi, kujichubua ngozi, kunyoa nyusi.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO MWEMA**



**PAUL KAJURUNGA JOHN.**

**MKUU WA SHULE.**

HEAD OF SCHOOL  
IGOTA SEC. SCHOOL  
P.O BOX 154 MAHENAE/ULANGA